**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KURUGENZI YA MAWASILIANO YA RAIS, IKULU**

*Dar es Salaam*
*18 Machi, 2026*

Baruapepe: press@ikulu.go.tz

# TAARIFA KWA UMMA

## RAIS SAMIA APOKEA RIPOTI YA TUME YA RAIS YA MABORESHO YA MFUMO WA KODI, AAHIDI UTEKELEZAJI WA MAPENDEKEZO KWA AWAMU

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, leo amepokea Ripoti ya Tume ya Rais ya Kutathmini Maboresho ya Mfumo wa Kodi nchini, katika hafla iliyofanyika Ikulu, Dar es Salaam.

Akizungumza wakati wa kupokea ripoti hiyo, Mheshimiwa Rais amesema uamuzi wa kuunda Tume hiyo ulitokana na haja ya kufanya tathmini ya kina ya mfumo wa kodi kufuatia malalamiko ya muda mrefu kutoka kwa wananchi, wafanyabiashara, wawekezaji na wadau wa maendeleo kuhusu changamoto zilizopo katika mfumo wa sasa.

Amesema tathmini kubwa ya mwisho ilifanywa na Tume ya Mtei kati ya mwaka 1989 na 1991, takribani miaka 35 imepita, hivyo kulikuwa na ulazima wa kuhuisha mfumo wa kodi ili uendane na mahitaji ya sasa ya kiuchumi, kiuwekezaji na kibiashara.

Mheshimiwa Rais ameeleza kuwa ripoti hiyo imekamilika katika kipindi ambacho dunia inapitia mabadiliko makubwa ya kiteknolojia, kiuchumi na kisiasa, hali inayozitaka nchi kuwa na sera thabiti na zinazotabirika pamoja na mifumo imara ya kitaasisi.

Amesisitiza kuwa mfumo bora wa kodi ni nyenzo muhimu katika kujenga uchumi imara, jumuishi na shindani, na katika kuiwezesha Serikali kukusanya rasilimali zinazohitajika kwa maendeleo ya Taifa na ustawi wa wananchi.

Aidha, Mheshimiwa Rais amesema maboresho ya mfumo wa kodi ni sehemu muhimu ya safari ya Tanzania kuelekea Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050, inayolenga kujenga uchumi imara unaoongozwa na uzalishaji, unaoshindana kimataifa na unaowanufaisha wananchi wengi zaidi.

Amesisitiza kuwa utekelezaji wa Dira hiyo unahitaji mchango wa mapato wa asilimia 22 kutoka Serikalini, asilimia 70 kutoka sekta binafsi na asilimia 8 kutoka mashirika ya umma, akibainisha kuwa, "Sekta binafsi lazima tuiwezeshe."

Mheshimiwa Rais ameipongeza Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), taasisi nyingine za ukusanyaji mapato, wafanyabiashara na wananchi kwa ujumla kwa kuendelea kuunga mkono jitihada za Serikali za kuongeza mapato kwa hiari na uzalendo.

Hata hivyo, amebainisha kuwa bado ipo fursa kubwa zaidi ya kuboresha mfumo kwa kuongeza ushiriki wa wananchi wengi zaidi katika uchumi rasmi, hasa wale waliopo katika sekta isiyo rasmi ili waweze kunufaika na fursa za mikopo, mitaji, masoko, maarifa na ushiriki mpana katika uchumi wa kisasa.

Mheshimiwa Rais amesema Serikali itayafanyia kazi mapendekezo yote 284 yaliyowasilishwa na Tume na itaandaa mkakati wa utekelezaji wa muda mfupi, wa kati na wa muda mrefu.

Amesisitiza dhamira hiyo kwa kusema, ***"Nimesikiliza kwa makini mapendekezo ya Tume yako 284. Tutayatekeleza."***

Ameongeza kuwa utekelezaji huo utahusisha uchambuzi wa kina, maandalizi ya kutosha na ushirikishwaji mpana wa wadau wote, akiongeza kuwa mabadiliko katika mfumo wa kodi ni jambo lisiloepukika.

***"Pamoja na changamoto za mfumo wa kodi, mabadiliko ni lazima na muhimu. Hata nyoka hujibadilisha, hujivua gamba. Sisi pia tunapaswa tubadilike,"*** amesisitiza.

Amefafanua kuwa lengo ni kuwa na mfumo wa kodi wenye usawa, utulivu na unaoeleweka kwa pamoja kati ya mtoza kodi na mlipakodi, usio na tafsiri kinzani, wenye sera isiyoegemea upande mmoja (neutral), kodi zisizoumiza, lakini zinazowezesha Serikali kupata mapato na biashara nazo kustawi.

Aidha, amesema Tanzania inalenga kufikia uwiano wa mapato ya kodi kwa Pato la Taifa wa asilimia 18 kama hatua muhimu kuelekea malengo ya muda mrefu ya maendeleo.

Kwa upande wake, Mwenyekiti wa Tume, Balozi Ombeni Sefue, amesema Tume imekamilisha jukumu lake kwa kuzingatia matarajio ya wananchi kuhusu mfumo wa kodi unaotakiwa na unaoendana na mazingira ya sasa.

Amesisitiza kuwa, ***"Hatuna budi kuwa na mfumo wa kodi unaopanua wigo wa kodi, na kuhakikisha kila mtu anachangia kadri ya kipato chake lakini kwa namna iliyo rahisi, wazi, ya haki na usawa."***

Ameeleza kuwa Tume imebaini changamoto kadhaa katika mfumo uliopo, zikiwemo viwango vikubwa vya baadhi ya kodi na tozo, udhaifu katika utatuzi wa migogoro ya kikodi, uratibu hafifu wa taasisi zinazokusanya mapato, pamoja na wigo mdogo wa walipakodi.

Katika kusisitiza umuhimu wa mageuzi ya kimkakati, amesema, ***"Bila mabadiliko makubwa, Tanzania itaendelea kukusanya kodi kutoka kwa wachache, tena kwa usumbufu."***

Balozi Sefue pia amesisitiza umuhimu wa kuweka mizani kati ya ukusanyaji wa mapato na ukuaji wa uchumi, akieleza kuwa, ***"Hatuwezi kuvuna bila kupanda; wala kukamua maziwa bila ng'ombe kulishwa,"*** akimaanisha kuwa mfumo wa kodi unapaswa kuimarisha uwekezaji na biashara ili kuongeza mapato kwa njia endelevu.

Kwa mujibu wa tathmini ya Tume, utekelezaji kamili wa mapendekezo yote unaweza kuongeza mapato ya Serikali kwa kiasi cha TZS trilioni 11.025 katika kipindi cha miaka mitatu ya mwanzo, na kuiwezesha nchi kufikia uwiano wa mapato ya kodi kwa Pato la Taifa wa asilimia 18.

Mheshimiwa Rais amehitimisha kwa kusisitiza kuwa mageuzi haya yanahitaji ushirikiano wa Serikali, sekta binafsi na wananchi wote, pamoja na utayari wa kubadilika ili kujenga mfumo wa kodi unaoendana na mahitaji ya Taifa na mabadiliko ya dunia.

Bakari S. Machumu
Mkurugenzi wa Mawasiliano ya Rais, Ikulu